


# MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA SERIKALI

*Kipindi cha Awamu ya 6*

# Bariadi DC







www. bariadidc.go.tz

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI

# MUHTASARI WA MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI(CCM) MWAKA 2020 – 2025 KWA KIPINDI CHA AWAMU YA SITA KUANZIA JANUARI 2021 HADI DESEMBA 2024

## 1. UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi ilianzishwa mwaka 1985 kwa tangazo la Serikali namba 17429/12-88 chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa na.7 na 8 ya mwaka 1982 kuhusu uanzishwaji wa mamlaka za Serikali za Mitaa. Sheria ilitoa mamlaka kwa Serikali za Mitaa kulinda na kuendeleza ustawi wa wananchi katika eneo husika.

Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi ilianzishwa baada ya mkoa wa Shinyanga kugawanywa, na Wilaya ya Bariadi kuwa sehemu ya Mkoa wa Simiyu. Awali Bariadi ilikuwa ni sehemu ya Mkoa wa Shinyanga. Kwa mujibu wa mabadiliko ya kiutawala yaliyotokea kati ya mwaka 2010 hadi 2013, Wilaya ya Bariadi iligawanywa kuwa Wilaya huru na kuanzisha Halmashauri yake ambayo baadae iligawanywa na kuwa Halmashauri tatu; Halmshauri ya Wilaya ya Bariadi, Halmashauri ya Mji wa Bariadi na Halmashauri ya Wilaya ya Itilima.



***Kituo cha Afya Matongo***

Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi ina ukubwa wa Kilomita za Mraba 5,921.29 sawa na hekta 592,129. Halmashauri hii ina jumla ya Kata 21, vijiji 84 na vitongoji 512, pia Halmashauri ina Idadi ya watu 383,385 kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2022. Halmashauri ina jimbo moja la uchaguzi ambalo ni jimbo la Bariadi linalochukua eneo lote la Halmashauri ya Wilaya na eneo lote la Halmashauri ya Mji wa Bariadi. Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi wanajishughulisha na shughuli za Kilimo, Ufugaji, Biashara na utoaji wa huduma au shughuli mbalimbali za kijamii.

Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi ilihamia Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji iliyopo Isenge kata ya Dutwa mwaka 2023. Kabla ya hapo Ofisi za Halmashauri zilikuwa katika eneo la Halmashauri ya Mji (Bomani).

## 2.0 MAFANIKIO KATIKA UTEKELEZAJI WA KISEKTA

### 2.1 SEKTA YA ELIMU

Katika kipindi cha uongozi wa awamu ya sita (Januari 2021, hadi Desemba,2024) Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi kupitia Sekta ya Elimu Msingi, Halmashauri imepokea jumla ya Tshs. 6,189,096,996 katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwa ni ujenzi wa shule mpya za msingi (4), ujenzi wa madarasa 91, ukamilishaji wa madarasa 120 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi, ujenzi wa bweni 1 la wanafunzi wenye mahitaji maalum na uzio, Ujenzi wa Nyumba 6 za waalimu na ujenzi wa matundu ya vyoo na mifumo ya maji 420



***Shule ya Sekondari Ihusi***



*Hospitali ya Wilaya*

Jedwali na. 1. Utekelezaji kwa msimu wa 2020/2021, 2021/2022, 2022/2023 na 2023/2024

| | 2020/2021 | | 2021/2022 | | 2022/2023 | | 2023/2024 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Lengo (Tani) | Halisi (Tani) | Lengo (Tani) | Halisi (Tani) | Lengo (Tani) | Halisi (Tani) | Lengo (Tani) (Tani) | Lengo (Tani) |
| Mahindi | 72,538 | 87,045.6 | 69,524 | 62,571.60 | 79,018.2 | 79,018.2 | 68,259 | 170,647.50 |
| Mpunga | 13,415 | 14,756.5 | 9,475 | 10,422.50 | 20,580.3 | 20,162.3 | 21,067 | 52,667.5 |
| Mtama | 9,783 | 9,783 | 8.804.7 | 5,482 | 8,180.7 | 6,194.4 | 5,284 | 8,982.80 |
| Maharage | 3,169 | 2,218.3 | 2,842 | 1,989.40 | 2,069 | 2,268 | 3,758.9 | 6,390.1 |
| Choroko | 13,967 | 10,475.3 | 15,661 | 11,745.80 | 11,599.5 | 10,791.8 | 13,962.5 | 30,717.5 |
| Dengu | 8,813 | 6,169.1 | 6,849 | 4,583.6 | 8,711 | 6,097.7 | 7,269.5 | 10,904.3 |
| Mbaazi | 2,142 | 1,927.8 | 1,271.50 | 1,082.5 | 11,599.5 | 10,791..8 | 3,907.5 | 7,034 |
| Muhogo | 1,409 | 9,863 | 227 | 1,816 | 11,599.5 | 10,791.8 | 1,362 | 34,050 |
| V/ Vitamu | 15,344 | 122,752 | 12,153 | 97,224 | 11,599.5 | 10,791.8 | 15,831 | 237,465 |
| Karanga | 3,861 | 3,088.8 | 4,338 | 3,470.40 | 11,599.5 | 10,791.8 | 2,963 | 5,333.40 |
| Alizeti | 8,923 | 5,353.8 | 7,491.4 | 5,457.3 | 15,949.5 | 16,909.5 | 13,749 | 34,372.5 |
| Pamba | 53,681 | 80,521.5 | 40,320 | 14,608 | 77,458.5 | 19,278.1 | 47,438 | 6,829 |

katika shule za msingi.

Aidha, kwa upande wa Elimu Sekondari, Katika kipindi cha uongozi wa awamu ya sita (Januari 2021, hadi Desemba,2024) Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi imepokea jumla ya Tshs. 8,777,290,057 katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwa ni ujenzi wa shule mpya 5 za Sekondari (Shule ya Sekondari ya Wasichana Simiyu, Ihusi Sekondari, Mwamoto Sekondari, Sekondari ya Amali na Gibishi Sekondari), ujenzi wa madarasa 68 katika Shule za Sekondari, ukamilishaji wa madarasa 23 katika Shule za Sekondari, ujenzi wa mabweni 7, ujenzi wa chumba cha Tehama, ujenzi wa nyumba 5 za walimu, ujenzi wa matundu 36 ya vyoo na Ujenzi wa maabara 10.

2.2 SEKTA YA AFYA

Katika kipindi cha uongozi wa awamu ya sita (Januari 2021, hadi Desemba,2024) Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi kupitia Sekta ya Afya, imepokea jumla ya Tshs. 3,300,610,347.20 katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo ikiwa ni ukamilishaji wa Zahanati 13 zikiwemo zahanati za Kilabela, Salaliya, Ikungulyandili,Mwadobana, Gilya, Nkindwabiye, Mwamondi n.k, Ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya zikiwemo wodi tano, jengo la upasuaji, nyumba na mtumishi na jengo la kuhifadhia maiti. Ujenzi wa vituo 3 vya Afya vya Miswaki, Matongo na Byuna. Ujenzi wa matundu 68 ya vyoo katika Zahanati na vituo vya Afya. Ujenzi wa nyumba 3 za watumishi na ununuzi wa vifaa tiba kwa ngazi ya Hospitali ya Wilaya, Zahanati na Vituo vya Afya, pamoja na utekelezaji wa Afua za Lishe.

2.3 SEKTA KILIMO

Kwa kipindi cha mwezi Januari 2021 hadi Desemba 2024, Halmashauri imeendelea kusimamia shughuli mbalimbali ikiwemo Ujenzi wa nyumba ya Afisa Ugani Kata ya Banemhi (Tshs. 40,000,000) pamoja na shughuli za kilimo ikiwa ni kusimamia ununuzi wa pamba mbegu ambapo Jumla ya Kampuni zilizoomba vibali vya kununua pamba mbegu zilikuwa ni kumi na sita (16) kikiwemo Chama Kikuu Cha Ushirika Mkoa wa Simiyu (SIMCU). Kusimamia shughuli za usambazaji na ukopeshaji wa mbegu za pamba ambapo jumla ya tani 1,056 zilikopeshwa kwa wakulima wa zao la pamba. Kuanzi- sha mashamba darasa matano (5) ya zao la mpunga katika Kata ya Sapiwi Kijiji cha Igegu Magharibi, Kata ya Ngulyati Kijiji cha Ngulya- ti, Kata ya Mwasubuya Kijiji cha Mwasubuya na Kata ya Kilalo Kijiji cha Kilalo. Pia, Halmashauri imeen- delea kutoa elimu kwa wakulima kuendelea na kilimo cha zao la pamba kwani zao la pamba hupand- wa kuanzia tarehe 15 Novemba hadi
15 Desemba kwa mujibu wa kalenda ya kilimo. Halmashauri imeendelea kutoa elimu kwa Wakulima kubaini kama kuna uwepo wa funza wa mahindi (Fall armyworm) ili kuweza kuwathibiti kabla madhara hayajawa makubwa.

Aidha katika mwaka wa fedha 2021/2022 serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Kilimo ilitoa vitendea kazi ambavyo ni Pikipiki ishirini na tatu (23) na pikipiki sita(6) zilitolewa na Bodi ya Pamba Tanzania kwa Maafisa Ugani kilimo katika Halmashauri ya Bariadi lengo likiwa ni kuwezesha utendaji kazi kwa Maafisa Ugani. Lakini pia Serikali ilitoa vitendea kazi kwa ajili ya kupima afya ya udongo lengo likiwa ni kuwasaidia Wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo

2.3.1 Kilimo cha Pamba

Msimu wa 2023/2024 wakulima



*Makao Makuu ya Halmashauri*



*Zahanati ya Mwadobana*

waliweza kulima kwa kiasi kikubwa na ekari za pamba zilizo limwa zilikuwa jumla ya ekari 118,595. Hata hivyo, Halmashauri inaendelea na zoezi la kubaina changamoto za wakulima ili kuendelea kutoa huduma kwa wakati ili kuweza kuongeza tija katika zao la pamba.

2.3.2 Hali ya Mazao na Uzalishaji

Kwa msimu wa 2023/2024 hali ya mazao ilikuwa ni ya wastani kutokana na mvua zilikuwa za wastani hivyo kufanya baadhi ya mazao kama mpunga, mahindi, mtama, choroko, mbaazi na maharage kuzalishwa kwa wingi isipokuwa uzalishaji wa zao la pamba ulishuka kutokana na mvua za vuli na masika kuwa nyingi iliyopelekea baadhi ya wakulima kushindwa kupanda na kupalilia mashamba yao. Kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini.

2.4 SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI

Katika kipindi cha mwezi Januari 2021 hadi Desemba 2024, Halmashauri katika kutekeleza majukumu ya Serikali imeendelea kutoa mafunzo kwa wafugaji kupitia mikutano zaidi ya 84 vijijini na kutembelea mfugaji mmoja mmoja. Jumla ya wafugaji 1,749 wamefikiwa na walipatiwa huduma na ushauri wa kitaalamu. Kufanya ukaguzi na vikao, na wamiliki wa maduka ya pembejeo na kuwapa elimu ya uendeshaji wa shughuli za biashara ya uuzaji wa pembejeo za Mifugo ambapo wafanyabiashara 43 wamepatiwa elimu husika. Ukaguzi wa leseni za biashara ya Samaki pamoja na vibali katika masoko yote yaliyopo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi umefanyika.

2.4.1 Chanjo ya Mifugo

Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi iliweza kufanya zoezi la chanjo ya ya homa ya mapafu ya Mifugo katika Vijiji 58 vya Tarafa ya Nkololo na Dutwa ambapo jumla ya ng'ombe 58,222 walichanjwa chanjo ya homa ya mapafu. Gharama ya chanjo ilikuwa ni Shilingi 1,000 kwa kila ng'ombe, hivyo mfugaji alipaswa kuchangia kiasi hicho cha fedha ili kusaidia uendeshaji wa zoezi hilo. Zoezi hili la chanjo linaendele.

2.4.2 Vitendea Kazi/Pikipiki

Pia Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliweza kutoa vitendea kazi aina ya pikipiki tano (5) ili kuwawezesha Maafisa Ugani na mifugo kuweza kuongeza ufanisi wa kazi kwa kuwatembelea Wafugaji na kutoa elimu na ushauri kuhusu ufugaji bora na wenye tija.

2.5 WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI (RUWASA)

Katika kipindi cha Januari 2021 hadi Desemba 2024, Ofisi ya RUWASA Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi imepokea jumla ya kiasi cha Tshs. 15,026,520,434.26, kwa ajili ya kuboresha huduma ya Maji kwa Wananchi wa maeneo ya Ibulyu, Ngulyati, Gambosi, Nyanguge na Kilalo. Upanuzi wa miundombinu ya maji Mwamlapa – Nduha, Mwasubuya, Ikungulyambeshi, Nkololo, Mwaubingi, Sapiwi, Ikungulyabashashi, Matongo na Masewa, hadi sasa upatikanaji wa maji umefika asilimia 75 kutokana na miradi iliyokamilika kutekelezwa kupitia Serikali ya awamu ya sita. Matarajio ya Serikali ni kufikia asilimia 85 ifikapo mwaka 2025, kama inavyopangwa.

2.6 WAKALA WA BARABARA (TARURA)

Katika kipindi cha Uongozi wa awamu ya sita (Januari 2021 hadi Desemba, 2024) TARURA kwa kushirikiana na Halmashauri ya wilaya ya Bariadi imepokea jumla ya kiasi cha Tshs. 8,198,167,135 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo Ujenzi wa Barabara zenye ukubwa wa kilomita 415.65 katika maeneo ya (Nkololo, Dutwa, Mwamondi, Igegu, Matongo, Gibishi ,Halawa, Gasuma, Mgodini, Ngulyai, Nyamswa ,Gambosi, Kilalo, Mwamlapa, Mwasubuya, Miswaki, Byuna , Nkindwabiye na Halawa) zenye thamani ya Tshs. 5,576,814,222. Ujenzi wa madaraja makubwa 2 yenye thamani ya Tshs. 1,451,424,912.5. Ujenzi wa madaraja ya mawe 20 yenye thamani ya Tshs. 536,928,000 na ujenzi wa kalavati 134 yenye thamani ya Tshs. 633,000,000.



*Mradi unaoendelea wa shule ya sekondari Mwamoto*

2.7 SHIRIKA LA UMEME TANESCO

Katika kipindi cha Uongozi wa awamu ya sita (Januari 2021 hadi Desemba, 2024) Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi kupiti Ofisi ya TANESCO imepokea kiasi cha Tshs.18,502,021,510 kwa ajili ya utekelezaji na kuboresha miundombinu ya umeme kwa mchanganuo ufuatao;-

Kupitia mkataba wa Rural Electricity Agency (REA) imepeleka huduma ya umeme kwa Vijiji 52 na Kata 21 kwa Tshs. 220,530,000. Pia, kupeleka umeme kwenye maeneo ya migodi ya wachimbaji wadogo wa dhahabu katika maeneo ya Nyawa, Halawa, Gasuma na Matongo kwa Tshs.18,047,490,962 na kupeleka umeme kwenye maeneo yasiyo na umeme (Network extension & Varous Customers) Katika maeneo ya Dutwa na Gambosi kwa kiasi cha Tshs. 234,000,548.

2.8 MATARAJIO YA MAENDELEO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI NI

i. Kuwa na Halmashauri yenye kutoa huduma bora na uwekezaji wa miradi kwa maendeleo endelevu
ii. Kutoa huduma bora na kuweka mazingira mazuri kwa uwekezaji kwa kutumia rasilimali zilizopo kiufanisi, kiufasaha na Utawala bora kwa maisha ya jamii.

3.0 HITIMISHO

Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo wananchi inaendelea kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikiwa ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025, kama ilivyoonekana katika mafanikio kwa kipindi cha Januari 2021 hadi Desemba 2024 katika kutekeleza shughuli mbalimbali za Halmashauri ya Wilaya Bariadi.